

Utoaji maziwa

Kiwango cha maziwa kinaongezeka wakati matawi ya viazi vitamu yanapolishwa kwa pamoja na mtama uliofunikwa kama inavyoonyeshwa hapa baadaye.

	Mtama pekee	Viazi pekee	Maziwa: (lita kwa siku)
Asili mia katika	100	0	10
Asili mia katika kila mgao	80	20	14

Maziwa hayo ya ziada yanaandamana na hali bora ya mwili.



Kenya Agricultural Research Institute

S.L.P. 5781 I, NAIROBI.
Simu: 254-20-4183301-20, Fax: 254-20-4183344
Baruapepe: resource.centre@kari.org
Tovuti: www.kari.org

Watayarishi:

Mugo, B.J. na Gatwiku, S.

Kwa maelezo zaidi, wasiliana na:


Mkurugenzi wa Kituo

KARILanet
S.L.P.1275-20100, Nakuru
Simu: (051) 85334/85324
Nukulishi: (051) 851268
Baruapepe: karilanet@africaonline.coke

Vijitabu za KARI za taarifa nambari / 43 / 2008

Shilingi 20 za Kenya

Chakula cha mifugo kutoka kwa mtama na matawi ya viazi vitamu



Utangulizi

Ulishaji wa mifugo ni tisho kubwa kwa wakulima wa maziwa wa nyanda za juu zilizo kavu nchini Kenya.

Kilimo na uhifadhi wa majani ya mtama wenye matumizi mengi ukichanganywa na matawi ya viazi vitamu ni baadhi ya suluhisho.

Mtama

Mtama wenye matumizi mengi una uwezo kuwapa mifugo chakula cha hali ya juu katika nyanda za juu. Hii ni kwa sababu:

- Mtama hustahimili hali za unyevu mbalimbali na hutoa chakula kingi wakati wa msimu wa kiangazi.



Mtama wenye matumizi mengi

Mtama ni wenye nishati nyingi lakini kiwango kidogo cha protini hivyo basi kuna haja ya kuongezea chakula chenye protini nyingi kama

vile matawi ya viazi vitamu. Matawi ya viazi vitamu hunawili vizuri katika nyanda za juu zilizo kavu na yanaweza kukuzwa mashambani. Yanaongezewa jinsi mifugo wanavyokula lishe hifadhi ya mtama na hivyo kuzidisha kiwango cha maziwa.



Matawi ya viazi vitamu

Lishe hifadhi ya mtama-viazi vitamu

Huu ni mseto wa mtama na matawi ya viazi vitamu na kuhifadhiwa na kugandishwa kwa njia za kawaida pasipokuwa na hewa ya mwai (oxygen).

Chakula cha mtama ni kizuri sana wakati mbegu zake zinakuwa ngumu. Kiwango cha urutubishi wake kinategemea utunzaji na hivyo basi ni muhimu kushughulikia vizuri.

Uhifadhi wa kufunikwa

Asilia zinazohitajika ni pamoja na:

- i) Karatasi ya plastiki (ukubwa utategemea shimo la kufunikia).
- iii) Kitu cha kufinyilia (pipa la maji).
- iii) Kikatio cha majani au kisu.

Hatua ya kwanza

Tayarisha shimo la kufunikia.

Hatua ya pili

Vuna mtama wakati mbegu ziko ngumu. Uvunaji mapema hufanya chakula kupoteza ladha na hivyo mlo mdogo.

Hatua ya tatu

Katakata sehemu ndogo ndogo za mtama ukitumia mashine kabla ya kuziba. Usitie nyongeza yoyote maana mtama huo una sukari zote zinazohitajika kugandisha.

Hatua ya nne

Weka chakula hicho kwa mpangilio na ufinyilie ili kuondoa hewa yoyote. Baada ya shimo kusheheni, funika kwa karatasi ya plastiki. Chakula hiki kiachwe kigande na kutumiwa wakati kuna uhaba wa chakula.